



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.S.20/86/Vol.II/55

25.04.2023

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kuomba nafasi ya Ajira za Makatibu Mhutasi kwa masharti ya kudumu. Tangazo hili ni baada ya kupokea vibali vya ajira mpya yenye Kumb.Na. FA.97/228/01'TEMP'/06 cha tarehe 06 April, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mchanganuo wa nafasi hizo ni kama ufuatao: -

#### **KATIBU MUHTASI DRJ. III - Nafasi 03** **(a) KAZI NA MAJUKUMU**

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- iii. Kusaidia kutunza taarifa, kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za mkuu wake na ratiba zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanya kazi na kumwarifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitaji katika shughuli za kazi hapo ofisini
- v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumwarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao
- vi. Kusaidia kupokea majalada na kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika
- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazo kuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi

**(b) SIFA ZA MWOMBAJI**

1. Kuajiriwa mwenye Elimu ya kidato cha Nne/ Sita.
2. Awe amehudhuria masomo ya uhazili na kutunukiwa astashahada ya uhazili na kufaulu mtihani wa daraja la tatu.
3. Awe amefaulu somo la hati mkato, ya maneno ya Kiswahili na kingereza maneno 80 kwa dakika moja.
4. Awe amepata mafunzo ya Compyuta kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti cha program za Windows, Microsoft office, Internet, E-mail na Publisher.

**(c) Ngazi ya Mshahara**

TGS. B1 : 450,000/= kwa mwezi

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE AMBAO**  
**NI LAZIMA KUZINGATIA**

- (a) Mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania
- (b) Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya Jinai
- (c) Awe hajawahi kufukuzwa au kupunguzwa kazi Serikalini
- (d) Maombi ni lazima yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, kuhitimu Elimu ya Sekondari (*Result Slips hazitakubaliwa*) na vyuo vya mafunzo au Taaluma.
- (e) Maombi ni lazima yaambatanishwe na picha mbili za "passport size" za hivi karibuni
- (f) Maombi ni lazima yaambatishwe na wasifu "Curriculum Vitae" zenyne mawasilisno ya uhakika, Anuani, barua pepe na namba za simu.
- (g) Awe na Umri wa miaka 18 na usiozidi miaka 45
- (h) Mwombaji awe hajawahi kuajiriwa Serikalini na kupata cheki namba.
- (i) Waombaji wenge vyeti vya kidato cha nne na cheti cha taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundu wa Taifa (NACTE)


Waombaji wote wenye sifa watume maombi yao kwenye anwani ifuatazo: -

**Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Meru,  
S. L. P 462,  
USA - RIVER.**

**Barua za maombi zinapokelewa kuanzia tarehe 25.04.2023 hadi tarehe 08.05.2022 saa 9.30 Alasiri.**

Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya [www.merudc.go.tz](http://www.merudc.go.tz) na mbao za matangazo katika Ofisi ya Makao Makuu ya Halmashauri na Ofisi za Vijiji na Kata zilizopo Halmashauri ya Meru.

Tangazo hili limetolewa na:



*Mwl. Zainabu J. Makwinya*  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**